

5.0 HITIMISHO

Soko huria linawezesha uwepo wa bidhaa na huduma kwa walaji. Hata hivyo, ili kuhakikisha malengo tarajiwa ya soko huria yanafikiwa, sheria zinatoa haki na wajibu wa walaji na wazalishaji; watoa huduma na waagizaji kuhakikisha bidhaa na huduma zinatolewa kwa ushindani ili kuleta tija kwenye soko na kuwepo kwa huduma na bidhaa zenye kukidhi matarajio ya walaji.

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

Kwa Maoni, wasiliana na Tume
kupitia anuani ifuatayo :

Katibu Mtendaji,
Tume ya kurekebisha Sheria
Tanzania ,

Jengo la Taaluma Na. 1,
Barabara ya Mkalama
S.L. P 1718
DODOMA
TANZANIA

Barua pepe: lrct@lrct.go.tz
Tovuti: www.lrct.go.tz



HAKI ZA WALAJI

1.0 UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kufanya mapitio na kutathimini utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia.

Katika kutekeleza jukumu hili, mwaka 2017 Tume ilifanya mapitio ya sheria zinazosimamia haki za walaji nchini na kutoa mapendekezo kwa Serikali.

2.0 NINI MAANA YA HAKI ZA WALAJI

Haki za walaji ni stahiki za watumiaji wa bidhaa na huduma zinazotolewa na Serikali au sekta biansi kwa ajili mahitaji ya mtumiaji na siyo kumpatia faida mzalishaji na mtoa huduma pekee.

Mtumiaji wa bidhaa au huduma ana haki ya kulindwa dhidi ya mienendo ya kibiashara isiyo ya haki na inayoathiri ubora wa bidhaa na huduma na kuhatarisha usalama wa afya ya mtumiaji.

3.0 HAKI ZA MLAJI

Haki za mlaji zinajumuisha haki zifuatazo:

3.1 Haki ya kupata taarifa kuhusu Bidhaa na huduma
Walaji wana haki ya kupata taarifa sahihi kuhusu ubora, kiwango na usalama wa bidhaa au huduma kutoka kwa mzalishaji au mtoa huduma.

3.2 Haki ya Uwepo wa Maelekezo kwenye bidhaa iliyosindikwa

Mlaji ana haki ya kupewa taarifa sahihi kuhusu bidhaa na huduma ili kujiridhisha kuhusu ubora na kipimo halisi cha bidhaa husika. Mzalishaji au muingizaji wa bidhaa anatakiwa kuweka maelekezo katika bidhaa kwa maandishi ya lugha ya Kiswahili au kiingereza yanayosomeka vizuri.

3.3 Haki ya Kurudisha Mali Hafifu au Mbovu

Mlaji ana haki ya kurudisha bidhaa na kupewa bidhaa nyingine au kurekebisha kama itagundulika bidhaa husika ina upungufu au haifai kwa matumizi ndani ya muda maalum uliyoonyeshwa kwenye bidhaa husika.

3.4 Haki ya kupata Matangazo Sahihi kuhusu bidhaa na Huduma

Mlaji ana haki ya kupata matangazo yaliyo sahihi kuhusu bidhaa na huduma inayotolewa. Matangazo yanayovutia walaji kununua bidhaa na huduma zisizoendana na uahalisia wa bidhaa au huduma au zisizoendana na thamani ya fedha walizolipa.

3.5 Haki ya kupata bidhaa na huduma Bora na Bei za Soko za Haki.

Mlaji ana haki ya kupata bidhaa na huduma bora zenye thamani ya fedha aliyolipa kununua bidhaa au kupata huduma. Bidhaa au huduma inayotolewa ambayo ni hafifu kwa ulinganifu wa bei ni kinyume na misingi ya thamani ya fedha. Hii inaweza kusababisha nchi kuwa jalala la bidhaa mbovu.

3.6 Haki ya kufidwa kwa bidhaa zilizo hafifu

Mlaji ana wajibu wa kukagua na kuchagua bidhaa bora. Pia mlaji ana haki ya kurudisha bidhaa mbovu au hafifu ili kupata bidhaa bora kwa matumizi.

4.0 WAJIBU WA MLAJI

Licha ya mlaji kuwa na haki zilizotajwa hapo juu, mlaji ana wajibu wa:

kufanya utafiti na kulinganisha bidhaa au huduma kabla ya kununua;
Kutoa taarifa sahihi ya bidhaa au huduma anayoitaka;
Kulipia gharama;
Kudai biashara ya haki;
Kutambua na kuuliza bei; ubora, vigezo na masharti ya huduma na bidhaa;
Kusoma na kufuata maelekezo;
Kufahamu madhara ya matumizi ya bidhaa na huduma hafifu;
Kuhakikisha ulaji au matumizi ya bidhaa na huduma hazina madhara kwa mazingira na zinalinda miundo mbinu katika eneo lake.